**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI**

**MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**664** **MITAALA NA UFUNDISHAJI**

**Muda: Saa 3.** **15th November 2000**

---

**Maelekezo.**

1. Karatasi hii ina sehemu **A**, **B** na **C.**
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu **A** na maswali **mawili (2)** kutoka sehemu **B** na swali **moja (1)** kutoka sehemu **C**.
3. Sehemu **A** ina alama 36, sehemu **B** ina alama 40 na sehemu **C** ina alama 24.
4. Vifaa vya mawasiliano na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
5. Andika **namba yako ya mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

maktaba.tetea.org
TETEA


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

## SEHEMU A (Alama 36)

Jibu maswali yote kwenye sehemu hii.

1. Eleza kwa kina maana ya upangaji wa mitaala katika mfumo wa elimu.
2. Tofautisha kati ya elimu rasmi na elimu isiyo rasmi kwa kuzingatia dhima zake katika malezi ya mwanafunzi.
3. Eleza faida tatu za kutumia mbinu shirikishi katika kufundisha.
4. Taja hatua kuu tatu zinazohusiana na utekelezaji wa mitaala shuleni.
5. Bainisha uhusiano uliopo kati ya malengo ya elimu na malengo ya somo.
6. Kwa nini ni muhimu mwalimu kupanga mazingira bora ya kujifunzia kabla ya kipindi?
7. Taja vipengele vinavyopaswa kuzingatiwa wakati wa kupanga mbinu za kufundishia.
8. Eleza umuhimu wa kufanya tathmini endelevu kwa wanafunzi darasani.
9. Eleza changamoto zinazoweza kumpata mwalimu wakati wa kutumia zana za kufundishia.

## SEHEMU B (Alama 40)

Jibu maswali mawili (2) tu katika sehemu hii.

10. Eleza kwa mifano jinsi malengo ya taifa yanavyoweza kuathiri muundo wa mitaala ya shule za msingi.
11. Fafanua umuhimu wa kupanga ratiba ya ufundishaji kwa walimu wa shule ya msingi.
12. Jadili jukumu la mwalimu katika kuhakikisha kuwa maudhui ya somo yanalingana na uwezo wa wanafunzi.
13. Eleza athari za kutotumia tathmini katika mchakato wa kufundisha na kujifunza.

## SEHEMU C (Alama 24)

Jibu swali moja (1) tu katika sehemu hii.

14. Jadili umuhimu wa kushirikisha jamii katika maendeleo ya mitaala ya shule.
15. Eleza namna mwalimu anavyoweza kutumia ubunifu wake kuboresha mbinu za ufundishaji.
16. Jadili nafasi ya teknolojia katika kukuza ufanisi wa kufundisha na kujifunza.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org